

Je, Chanjo za Kuzuia COVID-19 Zilijaribiwa kwa Akina Nani?

Aprili 14, 2021

Kabla ya matumizi ya chanjo kuidhinishwa, chanjo hiyo hujaribiwa kwa idadi kubwa ya watu ili kuthibitisha kuwa inafanya kazi na iko salama. Haya huitwa majaribio ya kimatibabu. Wanasayansi ambao walijaribu chanjo za kuzuia COVID-19 walijumuisha watu anuwai, pamoja na kiasi fulani cha watu wa rangi na kabila tofauti, katika uchunguzi wao.

Kwa nini chanjo zilijaribiwa kwa watu kutoka asili mbalimbali?

Ni jambo la maana kwamba uchunguzi wa chanjo ujumuishe watu wa kujitolea kutoka kwa watu ambao watapata chanjo hizo. Wanasayansi ambao walijaribu chanjo za kuzuia COVID-19 walijua kuwa watu wa rangi walikuwa katika hatari kubwa ya kuugua na kufa kutokana na COVID-19 kutokana na mambo kama vile vizuizi vya kupata huduma za afya, mapato, elimu, kazi, na makazi salama. Kwa hiyo, walifanya jitihada za kimakusudi kujumuisha watu wa rangi katika uchunguzi wao. Hilo litampa kila mtu nafasi ya kupata kinga dhidi ya maradhi ya COVID-19.


Je, idadi ya watu katika uchunguzi wa chanjo ilikuwa tofauti jinsi gani?

Wanasayansi walijaribu chanjo hizo za kuzuia COVID-19 (ambazo sasa zimeidhinishwa nchini Canada) kwa maelfu ya watu kutoka asili nyingi na makabila tofauti. Jedwali hili linaonyesha utofauti kati ya watu hao.

Jamii au kabila la kujitambulisha*	Chanjo ya Moderna	Chanjo ya Pfizer-BioNTech	Chanjo ya Johnson and Johnson	Chanjo ya AstraZeneca
Watu weupe	79%	83%	62%	79%
Watu weusi au Waafrika-Wamarekani/Wamarekani wenye asili ya Kiafrika	10%	9%	17%	8%
Waasia	5%	4%	4%	4%
Wenyeji wa eneo ("Wahindi Wa Marekani" au "Wenyeji Wa Asili Wa Alaska")	0.8%	0.5%	8%	4%
Watu Wa Asili Ya Hawaii au Wakazi Wa Visiwa Vya Pasifiki	0.2%	0.2%	0.3%	--
Watu Wa Jamii Mbalimbali	2%	2%	45%	--
Watu Wa Asili Ya Kihispania/Latini	21%	28%	45%	22%
Jamii Zingine	2%	--	5%	--
Hajaripotowa/hajjulikani	0.9%	0.6%	3%	--

*Hizi ndizo istilahi zilizotumika katika utafiti huo wa kisayansi.

Washiriki wengine walijitambulisha kuwa wa zaidi ya kabila moja au jamii.



Uchunguzi wa chanjo ya Moderna ulifanywa nchini Marekani na utafiti/uchunguzi wa chanjo ya BioNTech ukafanyika nchini Marekani, Ajentina, Brazil, Ujerumani, Afrika Kusini, na Uturuki.


Uchunguzi wa chanjo ya Johnson and Johnson ulifanyika nchini Marekani, Brazil, Afrika Kusini pamoja na nchi zingine tano katika Marekani ya Kilatini (Ajentina, Chile, Kolombia, Peru na Mexico).

Uchanganuzi wa tafiti mseto za chanjo ya AstraZeneca zilizofanywa katika vituo 88 nchini Marekani, Peru na Chile

Je, chanjo hizo zilifanya kazi kwa njia sawa katika vikundi tofauti vya kikabila na rangi?

Ndio, majaribio yalionyesha kwamba chanj zilikuwa na ufanisi katika kukinga dhidi ya maradhi ya COVID-19. Zilikuwa na ufanisi sawa katika watu wenye asili tofauti za rangi na kabila.

Kuanzia Aprili 14, watu kote ulimwenguni, zikiwemo Uchina, Mexico, Bangladeshi na Afrika Kusini, wamepokea **dozi million 825** za chanjo tofauti za kuzuia COVID-19.



Tunatumaini kwamba utafaidika kutokana na maelezo haya! Twakuomba yasambaze kwa upana, uyatumie kama hati kurekodi sauti au video, au uyatafsiri katika lugha zaidi ili kuwafahamisha wengine. Tafadhali hakikisha umetambua chanzo cha maelezo haya: Women's College Hospital, OCASI, TAIBU Community Health Centre na Refugee 613.

Toleo la Aprili 14, 2021

Taarifa katika barua hii imeidhinishwa na madaktari wa Canada: Meb Rashid MD, Profesa Msaidizi, Chuo Kikuu Cha Toronto; Vanessa Redditt, MD, Mhadhiri, Chuo Kikuu Cha Toronto; na Isaac I. Bogoch, MD, Profesa Mshirika, Chuo Kikuu Cha Toronto

